UNESCO
United Nations
Educational, Scientific and
Cultural Organization

TOLEO LA MESSENGER LA **TURATHI ZISIZOGUSIKA**

KITENGO CHA TURATHI ZISIZOGUSIKA
www.unesco.org/culture/ich

OCTOBA 2007 n° 8
ISSN 2071-7784





## Maafikiano 2003

KUIDHINISHWA NA MATAIFA KUFIKIA OCTOBA 8, 2007

1 ALGERIA
2 MAURITIUS
3 UJAPANI
4 GABON
5 PANAMA
6 UCHINA
7 JAMHURI YA AFRIKA YA KATI
8 LATVIA
9 LITHUANIA
10 BELARUS
11 JAMHURI YA KOREA
12 USHELISHELI
13 JAMHURI YA KIARABU YA SYRIA
14 UMOJA WA MILKI ZA KIARABU
15 MALI
16 MONGOLIA
17 CROATIA
18 MISRI
19 OMAN
20 DOMINICA
21 INDIA
22 VIET NAM
23 PERU
24 PAKISTANI
25 BHUTAN
26 NIGERIA
27 ICELAND
28 MEXICO
29 SENEGAL
30 ROMANIA
31 ESTONIA
32 LUXEMBOURG
33 NICARAGUA
34 CYPRUS
35 UHABESHI
36 BOLIVIA
37 BRAZIL
38 BULGARIA
39 HUNGARY
40 JAMHURI YA KIISLAMU YA IRAN
41 JAMHURI YA MOLDOVA
42 YORDANI
43 SLOVAKIA
44 UBELGIJI
45 UTURUKI
46 BUKINI
47 ALBANIA
48 ZAMBIA
49 ARMENIA
50 ZIMBABWE
51 CAMBODIA
52 JAMHURI YA YUGOSLAV YA MAKEDONIA YA AWALI
53 MOROCCO
54 UFARANSA
55 CÔTE D'IVOIRE
56 BURKINA FASO
57 TUNISIA
58 HONDURAS
59 SAO TOME AND PRINCIPE
60 ARGENTINA
61 PHILIPPINES
62 BURUNDI
63 PARAGUAY
64 JAMHURI YA DOMINICA
65 GUATEMALA
66 HISPANIA
67 KYRGYZSTAN
68 MAURITANIA
69 UGIRIKI
70 LEBANON
71 NORWAY
72 AZERBAIJAN
73 URUGUAY
74 SAINT LUCIA
75 COSTA RICA
76 VENEZUELA
77 NIGER
78 CUBA
79 MONACO
80 DJIBOUTI
81 NAMIBIA
82 YEMENI

# Kikao cha pili cha Kamati

Kikao cha pili cha Kamati ya serikali za nchi kuhusu Ulinzi wa Turathi za Tamaduni Zisizogusika ambacho kilifanyika katika kisiwa cha Odaiba kwenye ghuba la Tokyo kuanzia Septemba tarehe 3 hadi 7 mwaka huu, kilikuwa na ajenda ndefu. Ni kupitia kwa ukarimu wa wanachama wa Kamati, hususan uongozi bora wa Mhe. Bw. Seiichi Kondo ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati pamoja na mjumbe wa kudumu kutoka Ujapani aliyeko UNESCO, ambapo mkutano huo ulihitimishwa na maamuzi ya mwisho yaliyogusia karibu vipengele vyote vya ajenda kutolewa. Kamati ilitayarisha maamuzi mengi ya utendakazi yanayohitajika ili kutekeleza Maafikiano ya Turathi Zisizogusika. Kibali cha maamuzi hayo kitatolewa na kikao cha Mkutano Mkuu wa Mataifa Wanachama wa Maafikiano hayo. Inatarajiwa kwamba katika kikao cha pili cha Mkutano Mkuu mwezi wa Juni 2008, jumuiko hili litaweza kujadili na kuyakubali maamuzi yote yaliyopendekezwa na Kamati. Ni kufikia hapo ambapo Maafikiano hayo yataweza kufanya kazi, kukiwemo na rekodi za kwanza kuwekwa katika zile orodha mbili za turathi zisizogusika ambazo zimepangiwa kutayarishwa mapema mwaka wa 2009.

Kikao cha Tokyo kilithibitisha maongozi ambayo tayari yalikuwa yameteuliwa na Kamati katika kikao cha kwanza Algeria, na katika kikao cha kwanza kisichokuwa cha kawaida kilichofanyika Uchina kwenye mwezi wa Mei mwaka huu. Hili lina umuhimu mkubwa: Inaonyesha kuwa Maafikiano haya yatakuwa ya kiutendakazi, yatakaojihusisha na uhifadhi utakaofanywa au kufanyiwa jamii mbalimbali, makundi na watu binafsi ambao ndio wanaosanii, na kubadili maumbo ya usanii huku wakipitisha kwa vizazi turathi za kudumu. Kamati ilipokuwa ikijishughulisha na Maongozi ya Utendakazi, ilienda mbele zaidi kushughulikia yale yaliyohusu ufasiri wa Maafikiano



Reiko Yoshida © UNESCO

*Kikao cha Kamati*

kisheria kwani haya yalikuwa yameathiri nyaraka mbalimbali zilizotayarishwa na Afisi Kuu. Kutokana na hili basi, baadhi ya maamuzi yaliandikwa upya wakati wa kikao hicho. Majadiliano yalikuwa ya kina hasa katika siku za mwanzo za mkutano. Kamati iliwajibika kuunda vikundi vya kufanya kazi ili kurahisisha shughuli zake. Aidha, iliunda vikao viwili vidogo vilivyojihusisha na kazi mahsusi.

Kamati ilikubali kwa shauku pendekezo la Uturuki la kuandaa kikao cha kawaida kijacho mjini Istanbul mwishoni mwa 2008. Kabla ya tarehe hiyo, Kamati ingekutana tena katika kikao kisichokuwa cha kawaida. Ilifurahia kukubali kwa Bulgaria kuandaa kikao hicho mjini Sofia mwezi wa Februari, 2008. Kikao hicho kitaiwezesha Kamati kutayarisha ripoti yake ya kila mwaka wa pili itakayopelekwa kwa kikao cha Mkutano Mkuu, na kadhalika kukamilisha Maongozi ya Utendakazi ili kupata kibali cha Mkutano Mkuu.

*Rieks Smeets, Kitengo cha Turathi Zisizogusika*

### Washiriki katika mkutano wa Tokyo

Kikao cha pili cha kawaida cha Kamati kilihudhuriwa na takriban watu 150. Hawa waliwakilisha:

- Wanachama wa Kamati 22;
- Wengine 16 kutoka katika Mataifa Wanachama wa Maafikiano;
- Mataifa Wanachama wa UNESCO na wanachama washiriki 13; na
- Mashirika yasiyokuwa ya serikali, yakiwemo mengine 11.

### Tawi la Utendakazi jipya la Kamati

Mwishoni mwa kikao chake cha pili, Kamati ilichagua tawi la utendakazi jipya kuhudumu hadi mwishoni mwa kikao cha tatu cha kawaida ambacho kilipangwa kufanyika mwishoni mwa mwaka wa 2008 huko Istanbul.

**Tawi jipya la Utendakazi linajumuisha:**

- Mwenyekiti: Mhe. Bw. Faruk Logoglu (Uturuki)
- Manaibu Wenyekiti: Hungary, India, Mexico, Umoja wa Milki za Kiarabu
- Mwandishi wa Mkutano: Bi. Claudine-Augee Angoue (Gabon)

Vikao vya Kamati visivyo vya kawaida vitachagua tawi lao la utendakazi, kulingana na Kanuni ya 13 ya Kanuni za Kamati za Utendakazi.

(kushoto) *Zambia: Makishi Mascarade*
(kulia) *Nicaragua: El Güegüense*



© Zambia National Commission for UNESCO



© INC (Instituto Nicaragüense de Cultura)

## Maamuzi ya Utendakazi katika Orodha za Maafikiano

Taratibu zinazoelekea kuandikwa katika orodha mbili za Maafikiano – Orodha ya Ulinzi wa Haraka na Orodha Wakilishi- ziliafikiwa Tokyo zikisubiri kibali cha Mkutano Mkuu. Mataifa Wanachama pamoja na jamii mbalimbali zinasubiri kwa hamu ili kuona kule kurekodiwa kwa mara ya kwanza Turathi za Tamaduni Zisizogusika kwenye orodha hizo. Kulingana na Orodha Wakilishi, jamii na mataifa mbalimbali yangependa kushiriki ili kukuza turathi zao za kudumu ulimwenguni kote. Kulingana na ile Orodha ya Ulinzi wa Haraka, wanaona nafasi ya kuimarisha vito vya turathi hizo ambazo zinakabiliwa na matatizo. Huko Tokyo, Kamati ilitayarisha taratibu na ratiba za kupelekwa kwa majalada ya uteuzi, kuchunguzwa na kutathminiwa kwao, na mwishowe kurekodiwa na Kamati.

Kamati iliamua kwamba kipengele kimoja cha turathi zisizogusika hakiwezi kuwekwa katika orodha zote mbili kwa wakati mmoja, lakini Mataifa Wanachama husika yanaweza kuomba ili kito kimoja cha turathi kiweze kuhamishwa kutoka katika orodha moja hadi nyingine. Kamati pia ilitoa kauli kuwa ingependekeza kwa Mkutano Mkuu kwamba kito cha turathi ambacho hakitoshelezi kigezo kimoja au zaidi katika vile vigezo vinavyokiwezesha kurekodiwa kwenye orodha, kinaweza kuondolewa kutoka katika orodha hiyo. Ijapokuwa orodha zote mbili ziko wazi na kwamba nyingi ya taratibu zilizopendekezwa kufuatwa ili kurekodi kito zinafanana, Orodha ya Ulinzi wa Haraka ndiyo itakayopewa kipaumbele. Hapa pia taratibu za kurekodi zitakuwa na umakini zaidi.

## Mapendekezo ya Taratibu na Ratiba za Kurekodi turathi kwenye Orodha

Ijapokuwa zinafanana sana, taratibu na ratiba za orodha hizi mbili zinatofautiana kwa njia kadha. Uchunguzi wa kwanza wa uteuzi wa majalada yahusuyo Orodha ya Ulinzi wa Haraka itakuwa chini ya mamlaka ya mashirika ya umma au ya watu binafsi, wataalamu mahsusi au mashirika rasmi ya kutoa usaidizi ambayo yamechaguliwa na Kamati; haya yatatoa mapendekezo yao kwa Kamati hiyo. Mapendekezo ya kurekodiwa katika Orodha Wakilishi yatafuata utaratibu mwepesi ambapo yatachunguzwa na jopo dogo la Kamati ambalo pia litatoa mapendekezo yake. Mwishoni mwa taratibu hizi, Kamati itatathmini mapendekezo na maoni hayo na kuamua iwapo itarekodi kito cha turathi kilichopendekezwa.

Utaratibu unaohusu Orodha ya Ulinzi wa Haraka kwa kawaida utachukua miezi 18 (muda wa Mataifa yanayowasilisha maombi ya usaidizi wa kifedha ili kutayarisha majalada ni miezi 24). Hata hivyo, Kamati ilipendekeza ratiba mahsusi ili kwamba mkumbo wa kwanza wa uteuzi utapelekea kurekodiwa kwa turathi katika muda wa miezi 13 pekee. Kwa njia hii, rekodi za kwanza za orodha zote mbili zitatekelezwa Kamati itakapokutana mwishoni mwa 2009. Kuharakishwa kwa utaratibu uliopendekezwa kwenye rekodi za kwanza katika Orodha ya Ulinzi wa Haraka na kuwa na utaratibu wastani katika Orodha Wakilishi, yote yamewasilishwa hapa. (Kamati tayari ilikuwa imetoa vigezo vya kufuata ili kurekodi kwenye orodha hizo katika kikao cha mwezi wa Mei huko Uchina: *Tazama Toleo la Messenger no 7 la Turathi Zisizogusika.*

### Ratiba na Utaratibu Mahsusi uliopendekezwa katika Mkumbo wa Kwanza wa Kurekodiwa kwenye Orodha ya Ulinzi wa Haraka

**AWAMU 1: UTAYARISHAJI NA UWASILISHAJI**

| | |
|---|---|
| Julai 31 2008 | Tarehe ya mwisho kwa Mataifa Wanachama kutuma maombi ya ufadhili wa kifedha ili kutayarisha teuzi. |
| Oktoba 2008 | Tathmini ya maombi ya utayarishaji na Kamati |
| Machi 15 2009 | Tarehe ya mwisho ya teuzi kupokelewa na Afisi Kuu. Ikiwa uteuzi fulani umeonekana kutokamilika, Taifa Mwanachama litashauriwa kukamilisha. |
| Aprili 15 2009 | Tarehe ya mwisho kwa Mataifa Wanachama kuwasilisha habari zaidi zinazohitajika ili kukamilisha uteuzi, ikiwa zipo. |

**AWAMU 2: UCHUNGUZI**

| | |
|---|---|
| Aprili 2009 | Kamati kuchagua shirika moja au zaidi la ushauri. Taasisi za utafiti na/au wataalamu kuchunguza teuzi. |
| Aprili-Juni 2009 | Uchunguzi wa teuzi. |
| Juni 25 2009 | Tarehe ya mwisho kwa Mataifa Wanachama kuwasilisha habari zozote zaidi zinazotakiwa na wachunguzi ili kupitia vizuri uteuzi. |
| Julai 1 2009 | Afisi Kuu kupeleka ripoti za uchunguzi kwa Mataifa Wanachama yanayoteua. |
| Agosti 2009 | Afisi ya Utawala kupeleka ripoti za uchunguzi- pamoja na maoni ikiwa yapo, kutoka kwa Mataifa Wanachama hadi kwa Wanachama wa Kamati. |

**AWAMU 3: TATHMINI**

| | |
|---|---|
| Septemba 2009 | Kamati inatathmini teuzi na kuamua iwapo itarekodi vito vya turathi au la. |

### Ratiba na Utaratibu uliopendekezwa katika Mkumbo wa Kwanza wa Kurekodiwa kwenye Orodha Wakilishi

**AWAMU 1: UTAYARISHAJI NA UWASILISHAJI**

| | |
|---|---|
| Agosti 31 2008 | Tarehe ya mwisho ya teuzi kupokewa na Afisi ya Utawala. |
| Novemba 1 2008 | Tarehe ya mwisho kwa Afisi ya Utawala kushughulikia teuzi. Ikiwa uteuzi utaonekana kutokamilika, Taifa Mwanachama litashauriwa kuukamilisha. |
| Januari 15 2009 | Tarehe ya mwisho kwa Mataifa Wanachama kupeleka habari zozote za ziada zinazohitajika ili kukamilisha uteuzi. |

**AWAMU 2: UCHUNGUZI**

| | |
|---|---|
| Mei 2009 | Jopo dogo maalumu la Kamati kuchunguza teuzi. |
| Julai 1 2009 | Afisi ya Utawala kupeleka ripoti za uchunguzi wa jopo maalumu kwa Mataifa Wanachama yanayoteua. |
| Agosti 1 2009 | Afisi ya Utawala kupeleka ripoti za uchunguzi kwa wanachama wa Kamati. |

**AWAMU 3: TATHMINI**

| | |
|---|---|
| Septemba 2009 | Kamati kutathmini teuzi na kuamua iwapo itarekodi vito vya turathi au la. |

Yemen: Wimbo wa Sana'a

*Vidokezo vilivyotangazwa kama Vito vya Thamani Mapokezi ya mdomo na Turathi Zisizogusika za Kibinadamu vitaingizwa punde kwenye Orodha Wakilishi.*

*Vito vyote vya Thamanii, vikiwemo vile vilivyoonyeshwa hapa, vimewasilishwa kwenye wavuti mpya wa : http://www.unesco.org/culture/cih/ith/MasterpiecesV1.html*


© Samir Mokrani

## Kushirikishwa kwa vito vilivyotangazwa kama Vito vya Thamani kwenye Orodha Wakilishi

Kulingana na Kifungu cha 31 cha Maafikiano, Kamati iliamua kushirikisha vitu vyote vilivyotangazwa kama Vito vya Thamani vya Masimulizi ya mdomo na Turathi Zisizogusika za Kibinadamu kwenye Orodha Wakilishi mara tu baada ya Orodha hiyo kuanzishwa. Itafanya hivyo katika kikao chake cha tatu mwishoni mwa 2008. Orodha hiyo Wakilishi haitatofautisha kati ya Vito vya Thamani vya awali na vito vipya vilivyorekodiwa. Vyote vitajumuisha haki na masharti sawa. Mataifa yasiyo wanachama wa Maafikiano ambayo yana kito kimoja au zaidi cha Thamani katika maeneo yao, hayana budi kukubali kimaandishi masharti hayo. Aidha, yanaweza kuondoa vito vyao vya Thamani ili visishirikishwe katika Orodha hiyo. Utaratibu wa shughuli kama hii utatayarishwa katika kikao cha pili kisichokuwa cha kawaida Bulgaria (Februari 2008). Masharti hayo husika yatabainika tu baada ya Maamuzi ya Utendakazi kukubaliwa na kikao cha Mkutano Mkuu.

## Matumizi ya Hazina ya Turathi Zisizogusika

Kila baada ya miaka miwili Kamati itawajibika kuwasilisha pendekezo la matumizi ya Hazina kwa Mkutano Mkuu kupitia masharti yatakayotolewa na Mkutano huo. Huko Tokyo, Kamati ilianza kutayarisha masharti kama hayo ili yakubaliwe na Mkutano huo, huku ikipendekeza kwamba rasilmali ya Hazina hiyo itumiwe tu kwa usaidizi wa kimataifa. Aidha, Kamati ilikubali kuwa na mpango wa matumizi ya Hazina hiyo katika kipindi kinachoanza Juni 2008 hadi Juni 2010, kulingana na rasimu ya maelekezo. Pia ilipendekeza kwamba angalau asilimia 70 ya rasilmali iliyoko itumike kwa usaidizi wa kimataifa. Baki ya rasilmali hiyo ingetengewa shughuli mbalimbali, ukiwemo uhusika wa vikao vya Kamati vya wataalamu wanaowakilisha mataifa wanachama. Kadhalika, kuwe na uhusika wa mashirika na watu binafsi, wakiwemo wawakilishi wa jamii na makundi mbalimbali ambayo Kamati ingependa kuteua; na huduma za ushauri. Michango ya Mataifa Wanachama kwa Hazina inatarajiwa kuwa dola milioni 3 za Marekani kufikia Juni 2008.

## Uchaguzi na Ukuzaji wa Desturi Nzuri

Kwa mara nyingine tena, Kamati ilieleza umuhimu wa Kifungu cha 18 cha Maafikiano kinachoitaka kuchagua na kukuza desturi nzuri zaidi katika hifadhi za turathi. Aidha, ilisisitiza kwamba katika kutekeleza Kifungu hiki, uzingativu maalumu uwe katika mataifa yanayoendelea pamoja na ushirika unaohusisha sehemu za Kusini-Kusini na Kaskazini-Kusini-Kusini. Kamati inatarajia ukuzaji na usambazaji wa shughuli zilizoteuliwa uwe muhimu ili kuinua kiwango cha utambuzi juu ya umuhimu wa turathi zisizogusika kwa jumla, na kukuza ulinzi wazo. Wakati wa kujadili matumizi ya Hazina ya Turathi Zisizogusika, Kamati tayari ilikuwa imezingatia usaidizi wa matayarisho ambao Mataifa Wanachama yangepewa wakati wa kutayarisha mapendekezo yao chini ya Kifungu hiki, na kadhalika uwezekano wa kufadhili miradi na mipango baada ya kuchaguliwa. Kamati iliandika kwa kina Maongozi ya Utendakazi ambayo ikiwa yatakubaliwa na Mkutano Mkuu, yatatumika kama mwongozo wa kutekeleza shughuli hii muhimu.

## Usaidizi wa Kimataifa

Kamati ilitayarisha Maongozi ya kina kwa usaidizi wa kimataifa (Vifungu 19-24), ambapo maombi yatakayopewa kipaumbele yatahusisha:

- Uhifadhi wa turathi zilizorekodiwa katika Orodha ya Ulinzi wa Haraka;
- Mipango, miradi na shughuli zingine za kulinda;
- Utayarishaji wa hesabu ya vitu; na
- Utayarishaji wa usaidizi kwa Mataifa Wanachama ambayo yangependa kuwasilisha maombi ya kurekodiwa vito vyao kwenye Orodha ya Ulinzi wa Haraka, pamoja na mapendekezo ya kuchagua desturi bora zaidi katika kulinda.

Kuhusika kwa jamii katika utayarishaji wa mapendekezo na maombi, pamoja na utekelezaji wa shughuli zilizopendekezwa, ni kigezo muhimu cha Kamati kama yalivyo mahitaji maalumu ya nchi zinazoendelea na msimamo wa usambazaji wa usawa wa kijiografia.

## Usaidizi wa Ushauri, Utambuzi rasmi na Watazamaji

Kamati iliitaka Afisi Kuu kutayarisha orodha ya mashirika yasiyokuwa ya serikali na taasisi zisizolenga kupata faida ambazo zina uzoefu wa yaliyomo kwenye Maafikiano. Kitengo cha Turathi Zisizogusika bado kinaendelea kukusanya habari kuhusu mashirika kama hayo, kikishirikiana na Mataifa Wanachama wa Maafikiano, hususan kupitia kwa Wajumbe wao wa Kudumu katika UNESCO na


Frank Proschan © UNESCO

*Viet Nam: Nafasi ya Utamaduni wa Gong*

MCHAPISHAJI Kitengo cha Turathi Zisizogusika
Sekta ya Tamaduni, UNESCO
1 Rue Miollis
75732 Paris Cedex 15, Ufaransa
Barua pepe: ich@unesco.org
Kipepesi: +33 (0) 145685752

MHARIRI MKUU Rieks Smeets

JOPO LA UHARIRI Fernando Brugman, Armelle Gaulier, Jana Gough, Oda Lehman, Fleur Perrier, Frank Proschan, David Stehl

*Toleo la Messenger kuhusu Turathi Zisizogusika* linapatikana katika umbo la chapa na elektroniki kwa Kiingereza, Kifaransa, Kihispania na Kiarabu.

Nakala ya Kiarabu imewezeshwa kupitia kwa mchango wa kifedha wa Mamlaka ya Utamaduni na Turathi ya Abu Dhabi, Milki ya Abu Dhabi – U.A.E.

Yote yaliyomo yanaweza kupakuliwa katika (www.unesco.org/culture/ich) na kupigwa chapa bila malipo ilimradi mwandishi atambuliwe.



© Conselho das Aldeias Waiãpi-Apina

turathi zisizogusika

## AJENDA

**NOVEMBA 29–30 2007**
"Mkutano wa Wataalamu kuhusu Mitindo ya kisasa katika kutayarisha Ramani ya Kiisimu", kwa matayarisho ya toleo la tatu la Ramani ya Lugha za Ulimwengu zilizo katika Hatari ya Kutoweka. Paris, Ufaransa.

**DISEMBA 11–13 2007**
Mkutano wa Kimaeneo kuhusu "Ulinzi wa Turathi Zisizogusika na Utalii Endelevu wa Kitamaduni: Nafasi na Changamoto", uliotayarishwa na Afisi ya UNESCO iliyoko Bangkok ikishirikiana na mpango wa uanzishaji wa Kituo cha Turathi Zisizogusika wa Asia-Pacific, Seoul. Hue, Viet Nam.

**DISEMBA 12–14 2007**
Mkutano wa maeneo madogo juu ya uimarishaji wa Maafikiano kuhusu Ulinzi wa Turathi Zisizogusika katika Pacific. Nadi, Fiji.

**FEBRUARI 2008**
Kikao cha pili kisicho cha kawaida cha Kamati ya serikali za nchi kuhusu Ulinzi wa Turathi za Tamaduni Zisizogusika. Sofia, Bulgaria.

**JUNI 2008**
Kikao cha pili cha kawaida cha Mkutano Mkuu wa Mataifa Wanachama wa Maafikiano kuhusu Ulinzi wa Turathi za Tamaduni Zisizogusika, Paris, Ufaransa.

**MWISHONI MWA 2008**
Kikao cha tatu cha kawaida cha Kamati ya serikali za nchi kuhusu Ulinzi wa Turathi za Tamaduni Zisizogusika. Istanbul, Uturuki.

Tume zao za Kitaifa. Habari zitahifadhiwa na kutayarishwa kila mara katika hazina data iliyotayarishwa na kitengo hicho. Hazina data hiyo itakuwa chini ya mamlaka ya Kamati kuweza kufanya lolote ilitakalo kutegemea sababu yoyote itakayofikiria muhimu kufanya hivyo.

Kamati pia iliamua juu ya majukumu ya yale mashirika yasiyokuwa ya serikali ambayo itayapendekeza kwa Mkutano Mkuu kwa lengo la kuyashirikisha kirasmi, na utaratibu wa kufanya hivyo. Kamati ilionelea kwamba majukumu yaliyopendekezwa kwa mashirika hayo yasiyokuwa ya serikali pia yangeweza kutekelezwa na mashirika mengine yenye ujuzi, pamoja na watu binafsi. Katika mwelekeo huu, Kamati iliunda tawi ambalo lingetayarisha makala kwa minajili ya kikao kijacho ili kuona kama mipango ingeimarishwa ya kuzihusisha jamii au wawakilishi wao, wajuzi, wataalamu, vituo vya kitaalamu na taasisi za utafiti katika utekelezaji wa Maafikiano. Aidha, ilizungumzia kwa kirefu juu ya uwezekano wa kushirikisha watazamaji katika mikutano yake. Baadaye iliamuliwa kwamba jambo hili lingejadiliwa zaidi katika kikao kijacho. Kwa wakati huo, Kamati ilikaribisha Mataifa Wanachama kuwasilisha majina ya mashirika yasiyokuwa ya serikali ambayo yangeshiriki kama watazamaji katika mkutano huo. Uamuzi huo pia unamruhusu Mwenyekiti wa Kamati kumuuliza Mkurugenzi Mkuu kuyaalika mashirika yaliyotajwa na Mataifa Wanachama, pamoja na yale yaliyo katika orodha ya Afisi ya Utawala ili kuhudhuria mkutano ujao kama watazamaji.

## Nembo ya Maafikiano

Kamati maalumu kati ya serikali za Mataifa Wanachama iliamua kwamba Maafikiano yalihitaji nembo ili kujulikana zaidi katika turathi zisizogusika na hifadhi yazo. Nembo hii itachaguliwa kupitia kwa mashindano ya wazi ya kimataifa, huku yakisimamiwa na jopo litakaloundwa na Kamati. UNESCO sasa inatangaza shindano la kuchora nembo ambayo itaakisi malengo na kiini cha Maafikiano.

UNESCO inakaribisha maombi kutoka kwa wataalamu na wanagenzi katika sanaa ya uchoraji, wana sanaa na wajuzi wa turathi za tamaduni zisizogusika kutoka katika Mataifa yote Wanachama. Kila mshiriki anaweza kuwasilisha mchoro mmoja, ikiwemo nakala nyeusi-nyeupe na ya rangi. Muda wa makataa wa kuwasilisha michoro hiyo kwa UNESCO ni Februari 15, 2008.

Masharti na taratibu za shindano hili pamoja na fomu ya kutuma maombi zinapatikana kwenye wavuti wa shindano: www.unesco.org/culture/ich/en/emblem/
Kwa habari zaidi, andika kwa ICH-emblem@unesco.org

Katika kikao chake cha tatu huko Istanbul, Kamati itachagua mchoro ulioshinda na kutuza zawadi ya dola 15,000 za Marekani. Mchoro huo ndio utakaotumika kama nembo rasmi ya Maafikiano.

***Kwa maamuzi yaliyotolewa Tokyo, ripoti ya mwandishi ya mkutano huo, orodha ya washiriki, nyaraka awali za utendakazi na – katikati ya Novemba – muhtasari wa rekodi ya kikao cha Tokyo, tazama http:www.unesco.org/culture/ich/en/2COM/***



*Michoro ya Mchanga ya Vanuatu*

© Vanuatu National Cultural Council